TANGAZO LA SERIKALI NA. 195 la tarehe 6/3/2020

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*Imetungwa chini ya Kifungu cha 6(1) na 16(1)*

SHERIA NDOGO YA USHURU WA ZAO LA MKONGE) YA HALMASHAURI YA MJI WA HANDENI YA MWAKA, 2020

Jina na tarehe ya kuanza

1. Sheria ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ushuru wa zao la Mkonge ya Halmashauri ya Mji wa Handeni ya Mwaka, 2020 na itaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Mji wa Handeni.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Mji wa Handeni;

"kibali" ni idhini ya maandishi inayotolewa na Halmashauri kwa muuzaji, mnunuzi, kampuni, asasi ama mtu yeyote anayekusudia kusafirisha zao la Mkonge kwenda nje ya eneo la Halmashauri;

"Mkonge" maana yake ni majani au singa au nyuzi zitokanazo na mmea wa Mkonge;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri au Afisa yeyote wa Umma atayeteuliwa kukaimu nafasi ya Mkurugenzi;

"mlipa ushuru" maana yake ni mtu binafsi, kikundi cha biashara, kampuni, shirika au vyama vya ushirika vya msingi vya mazao yenye leseni ya biashara ya kununua Mkonge unaotoka ndani ya Halmashauri ambaye anawajibika kulipa ushuru wa mazao chini ya Sheria Ndogo hii;

"mnunuzi" maana yake ni kampuni binafsi, vyama vya ushirika vya msingi vya mazao au mtu yeyote mwenye leseni ya biashara ya kununua Mkonge;

"Wakala" maana yake ni mtu yeyote , taasisi au kikundi cha watu ambao wana Mkataba na Halmashauri wa kukusanya mapato ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii;

Utozaji wa Ushuru

4. Halmashauri itatoza ushuru wa zao la Mkonge kwa kiwango cha asilimia tatu ya bei ya mauzo kutoka kwa kila mnunuzi wa zao hilo kwenye eneo la Halmashauri.

Usafirishaji wa Mkonge

5.-(1) Mtu ye yote hatoruhusiwa kusafirisha Mkonge kutoka nje ya eneo la Halmashauri bila ya kuwa na kibali kitakachotolewa na Halmashauri.

(2) Mtu ye yote anayetaka kusafirisha Mkonge atatakiwa kuomba kibali kwa kujaza fomu maalum itakayopatikana katika ofisi ya Halmashauri.

(3) Halmashauri itatoa kibali cha kusafirisha Mkonge kwa mwombaji ndani ya siku saba toka tarehe ya maombi kuwasilishwa na kupokelewa Halmashauri.

Wajibu wa mnunuzi

6. Kila mnunuzi atakuwa na wajibu wa:-

(a) kulipa ushuru wa asilimia tatu ya bei ya mauzo kwa Halmashauri au wakala;

(b) kupokea stakabadhi ya kielektoniki ya malipo ya ushuru kutoka kwa Halmashauri au wakala;

(c) kuomba kibali cha kusafirisha Mkonge kwenda nje ya eneo la Halmashauri; na

(d) kuomba leseni ya kununua Mkonge katika eneo la

Halmashauri itakayotolewa na Halmashauri.

Uwezo wa kukagua na kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo

7. Kwa madhumuni ya usimamizi wa Sheria Ndogo hii, Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika eneo lolote la Halmashauri kwa ajili ya;-

(a) kukagua kumbukumbu na taarifa zinazohusu shughuli za mauzo ya Mkonge kwa lengo la kujua kiasi ambacho mlipa ushuru anastahili kulipa; na

(b) kukagua na kujiridhisha kama kiasi cha Mkonge kilichoombewa na kukatiwa kibali cha kusafirishwa nje ya Halmashauri kiko sawa au kinalingana na kiasi halisi kinachosafirishwa.

Makosa na Adhabu

8.-(1)Mtu ye yote atakuwa ametenda kosa endapo;

(a) atamzuia au atajaribu kumzuia Mkurugenzi au Afisa Mwidhiniwa kutekeleza wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hii;
(b) atamshawishi mtu mwingine kumzuia Mkurugenzi au Afisa Mwidhiniwa kutekeleza wajibu wake Sheria Ndogo hii;
(c) atasafirisha zao la Mkonge kutoka ndani ya Halmashauri kwenda nje ya eneo la Halmashauri bila ya kibali;
(d) atajihusisha na biashara ya Mkonge bila kuwa na leseni ya ununuzi wa Mkonge inayotolewa na Halmashauri;
(e) atakwepa au kushindwa kulipa Ushuru wa zao la Mkonge chini ya Sheria Ndogo hii;
(f) atakataa bila sababu za msingi kutoa taarifa zinazohitajika kwa Mkurugenzi au Afisa Mwidhiniwa zinazohusu ushuru wa zao la Mkonge;

Adhabu

(2) Mtu ye yote atakayetiwa hatiani kwa kukiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) atahukumiwa adhabu ya faini isiyopungua shilingi Laki Mbili na isiyozidi shilingi Milioni Moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote kwa pamoja.

Kufifilisha kosa

9. Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 8, Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii kiasi cha shillingi laki moja ikiwa mtu huyo atakiri kosa kwa maandishi kwa kujaza fomu iliyoambatishwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hii na kuwa tayari kutimiza wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hii.

JEDWALI

HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

*(Chini ya kifungu cha 9)*

Mimi ……………………………………………………………..nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ……………………………………………………….ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Handeni, kwamba tarehe………………ya mwezi …………………………mwaka…………………………………nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha ………………..cha Sheria Ndogo ya Ushuru za Zao la Mkonge ya Halmashauri ya Mji wa Handeni ya Mwaka 2020.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri, niko tayari kutimiza wajibu wangu chini ya Sheria Ndogo hii..

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWAHIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe…………. ya Mwezi………………………………… Mwaka ……………………

*Jina………………………………………………….. Saini…………………..…………………….*

Mbele ya:-

Jina: ……………………………………………Cheo: …………………………………………………

Saini: ……………………………

Muhuri ya Halmashauri ya Mji Handen ulibandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Baraza la madiwani uliofanyika tarehe 27 mwezi Disemba, 2019 mbele ya:-

……………………………………….
KENNETH K. HAULE,
*Mkurugenzi*
*Halmashauri ya Mji Handeni*

**L. S**

………………………………………..
TWAHA ALLY MGAYA,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Mji* Handeni

NAKUBALI

Dodoma
5 Machi, 2020

MHE. SELEMANI JAFFO (MB.),
*Ofisi Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa*